**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TAARIFA KWA UMMA**
**KUHUSU UTEUZI WA MBUNGE NA DIWANI MWANAMKE WA**
**VITI MAALUMU**

**Dodoma, 30 Januari, 2026**

Kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 78(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ikisomwa pamoja na kifungu cha 112 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais Wabunge na Madiwani, Sura ya 343, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake kilichofanyika tarehe 30 Januari, 2026 imefanya uteuzi wa **Ndugu BENG'I MAZANA ISSA** wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa Mbunge Mwanamke wa Viti Maalumu.

Nafasi hiyo imetokana na kifo cha **Ndugu HALIMA IDD NASSOR** aliyekuwa Mbunge Mwanamke wa Viti Maalumu kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilichotokea tarehe 18 Januari, 2026.

Aidha, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 25(1)(c) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288 kikisomwa pamoja na kifungu cha 113 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sura ya 343, Tume katika kikao hicho imefanya uteuzi wa **Ndugu IRENE LINUS MWANGARA** wa Chama Cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) kuwa Diwani Mwanamke wa Viti Maalumu katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Uteuzi huo umefanyika baada ya kukamilika kwa uchaguzi wa marudio katika Kata ya Mzinga, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ambapo uchaguzi uliahirishwa kutokana na kifo cha mgombea katika kata husika.

Imetolewa na:

Kailima, R. K
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**